**HOTUBA YA IJUMAA**

**منزلة الشهداء عند ربهم**

**Nafasi ya Mashahidi kwa Mola wao**.

Imefasiriwa

na

profesa Ayman Alasar

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote Mwenye kuzungumza ndani ya Kitabu chake Kitukufu:

**وَلا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاء عِندَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ * فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِمْ مِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ * يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ.**

{**Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi * Wanafurahia aliyo wapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake, na wanawashangilia wale ambao bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika * Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi malipo ya Waumini**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad S.A.W ni Mtume wake na mja wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na kwa Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

Baada ya utangulizi:

Mtu aliyefariki shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ana nafasi ya juu kabisa na ukaribu uliomtukufu, huo ushahidi ni umeteuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mashujaa waliojitoa kwa nafsi zao katika njia ya kutetea haki na

kuilinda, wakiwa na utashi mkubwa wa kulinda nchi na usalama kwa watu wake na ardhi yake, ambapo Mola Mtukufu Anasema: **وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَيَتَّخِذَ مِنْكُمْ شُهَدَاءَ** {**ili Mwenyezi Mungu awapambanue walio amini na awateuwe miongoni mwenu mashahidi**}.

Hivyo basi Mwenyezi Mungu amehusisha Mashahidi nafasi ya juu na ubora mkubwa pamoja na karama za pekee, na dalili kubwa ya hilo ni kauli ya Mtume: **وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوَدِدْتُ أَنِّي أُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللهِ ثُمَّ أُحْيَا، ثُمَّ أُقْتَلُ ثُمَّ أُحْيَا، ثُمَّ أُقْتَلُ ثُمَّ أُحْيَا، ثُمَّ أُقْتَلُ** "*Ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, natamani mimi ningeuliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha nikarudishiwa uhai, kisha nikauwawa kisha nikarudishiwa uhai kisha nikauwawa kisha nikarudishiwa uhai*".

Miongoni mwa nafasi ya Shahidi: Ni kuwa wao wapo hai kwa Mola wao ni uhai unaozidia akili na uelewa wa mwanadamu, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

**وَلا تَقُولُواْ لِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبيلِ اللّهِ أَمْوَات بَلْ أَحْيَاء وَلَكِن لاَّ تَشْعُرُونَ .**

{**Wala msiseme kuwa wale walio uwawa katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni wafu; bali hao ni wahai, lakini nyinyi hamtambui**}, na kutoka kwa Jabiri Ibn Abdillah R.A amesema: Nilikutana na Mtume S.A.W akaniambia: Ewe Jabir una nini nakuona unahuzuni? Nikasema: Ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwani baba yangu amefariki akiwa shahidi na ameacha watoto na deni. Mtume akasema: Je nikubasharia kile alichokutana nacho baba yako? Nikasema: Ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume akasema: Mwenyezi Mungu hajawahi kuzungumza na mtu yeyote isipokuwa kwa nyuma ya uzio, amemrejeshea uhai baba yako na akazungumza naye bila ya uzio, akasema kumwambia: Ewe mja wangu unatamani nini nikupe, akasema: Ewe Mola nipe tena uhai nikapigane tena kwa ajili yako. Mola Mtukufu Akasema: Tayari kauli yangu imeshatangulia kuwa wao huko duniani hawatarejea tena, anasema ndio ikateremka Aya hii:

**وَلا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاء عِندَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ.**

{**Wala kabisa usiwadhanie walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi**}, kwa vile watu

mashahidi wapo hai mbele ya Mola wao Mtukufu basi pia wapo hai katika kumbukumbu za nchi, kwani haiwezi kusahaulika ushujaa wao kwa muda kupita.

Na nafasi pia ya Mashahidi: Ni kuwa roho zao ni zenye kuneemeshwa kwa Mola wao Mtukufu, zinatembeatembea Peponi kama zinavyotaka, ambapo Mtume SAW anasema:

**لَمَّا أُصِيبَ إِخْوَانُكُمْ بِأُحُدٍ، جَعَلَ اللَّهُ أَرْوَاحَهُمْ فِي جَوْفِ طَيْرٍ خُضْرٍ، تَرِدُ أَنْهَارَ الْجَنَّةِ، تَأْكُلُ مِنْ ثِمَارِهَا، وَتَأْوِي إِلَى قَنَادِيلَ مِنْ ذَهَبٍ مُعَلَّقَةٍ فِي ظِلِّ الْعَرْشِ.**

“*Pindi ndugu zenu walipouwawa katika vita vya Badri Mwenyezi Mungu akaziweka roho zao ndani ya miili ya ndege wa kijani wakiwa wanatembea nazo kwenye mito ya Peponi na kula matunda yake na wanarudi kwenye makazi yao yaliyopo chini ya Arshi*”.

Na miongoni mwa nafasi zao pia: Ni kuwa wao ni watu wenye malipo makubwa na wenye nuru siku ya Kiyama, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

**وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ لَهُمْ أَجْرُهُمْ وَنُورُهُمْ.**

{**Na Mashahidi mbele ya Mola wao Mlezi. Wao watapata malipo yao na nuru yao**}. Na Mtume SAW anasema kumwambia Mama wa Harithah Ibn Suraqah R.A pindi alipomuuliza kuhusu mwisho wa Harithah R.A na alikuwa amefarikia akiwa Shahidi kwenye vita vya Badri: “Ewe Mama Harithah mwanao amepata Pepo ya juu ya Firdausi”.

Miongoni mwa nafasi zao pia: Ni kuwa wao watapewa nafasi ya uombezi kwa ndugu zao siku ya Kiyama ikiwa ni malipo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kutokana na malezi yao mema kwao na kuwaandaa kwao, ambapo Mtume S.A.W anasema: **يَشْفَعُ الشَّهِيدُ فِي سَبْعِينَ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ** “*Aliyekufa Shahidi atapewa nafasi ya uombezi kwa watu sabini miongoni mwa ndugu zake*”.

Pia katika nafasi yao: Ni kuwa wao malipo yao yanayotokana na matendo yao hayakatiki bali yanaongezeka, ambapo Mtume S.A.W anasema:

كُلُّ مَيِّتٍ يُخْتَمُ عَلَى عَمَلِهِ إِلاَّ الَّذِي مَاتَ مُرَابِطًا فِي سَبِيلِ اللهِ فَإِنَّهُ يُنْمَى لَهُ عَمَلُهُ إِلَى يَوْمِ القِيَامَةِ، وَيَأْمَنُ مِنْ فِتْنَةِ القَبْرِ.

"*Kila mtu aliyefariki matendo yake mema hufikia mwisho isipokuwa yule ambaye amefariki katika njia ya Mwenyezi Mungu huyo matendo yake yanakuwa mpaka siku ya Kiyama, na mwili wake hukingwa na fitina za kaburini*".

****

**HOTUBA YA PILI.**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa nafasi ya Mashahidi anastahiki nayo Shahidi wa kweli ambaye amefahamu haki na akatakasa nia yake kwa ajili ya haki hiyo pamoja na kuilinda, akajitoa muhanga kwa ajili ya haki, na Shahidi wa kweli ni yule aliyefariki akiwa analinda na kutetea ardhi yake heshima yake nchi yake na usalama wa watu wake, ambapo Mtume S.A.W anasema:

مَنْ قُتِلَ دُونَ مَالِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ، وَمَنْ قُتِلَ دُونَ أَهْلِهِ، أَوْ دُونَ دَمِهِ، أَوْ دُونَ دِينِهِ فَهُوَ شَهِيدٌ .

"*Mwenye kuuwawa kwa ajili ya mali yake basi huyo anakufa Shahidi, na mwenye kuuwawa kwa ajili ya kutetea familia yake na ndugu zake au kwa ajili ya kulinda damu yake au kwa ajili ya dini yake basi huyo anakufa akiwa Shahidi*".

Tunasisitiza kuwa kuzitendea haki roho za Mashahidi wetu kunahitajika kwetu kuwa askari wa nchi yetu hii kubwa kwa kila mmoja kwa nafasi yake, na kila mmoja wetu anapaswa kufanya juhudi kubwa katika kuihudumia nchi yake, akiwa mwenye kutegemea malipo ya kufa Shahidi mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo Mtume S.A.W anasema:

مَنْ سَأَلَ اللَّهَ الشَّهَادَةَ بِصِدْقٍ بَلَّغَهُ اللَّهُ مَنَازِلَ الشُّهَدَاءِ وَإِنْ مَاتَ عَلَى فِرَاشِهِ.

“*Mwenye kumuomba Mwenyezi Mungu kwa kweli afe akiwa Shahidi basi Mwenyezi Mungu anamfikisha nafasi ya Mashahidi hata kama atafia kitandani kwake*”.

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba uilinde nchi yetu ya Misri pamoja na nchi za Kiislamu na Kiarabu.

Amin.